

OFISI YA RAIS (OR)

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

HALMASHAURI YA MANISPAA TABORA

SHULE YA SEKONDARI FUNDIKIRA,

S. L. P 799,

TABORA.

.../.../2020

MKUU WA SHULE,

SIMU NA: +255 (0) 756075682

KATA YA KILOLENI

MTAA WA MILAMBO

E-mail: [Fundikira@gmail.com](mailto:Fundikira@gmail.com)

Kumb Na. FSS/S/ 1/2939/JOIN/15

Jina la Mwanafunzi .....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI FUNDIKIRA  
HALMASHAURI YA TABORA MANISPAA MKOA WA TABORA MWAKA 2020**

**1.0 Utangulizi**

Ninayofuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Fundikira **2020**. Shule ya sekondari Fundikira ipo mtaa wa Milambo kata ya Kiloleni na kutokea Halmashauri ya manispaa ya Tabora ni umbali wa kilomita tano (05) Muhula wa kwanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/01/2021** ndani ya siku saba (**07**) uwe umeripoti.

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1 Sare za shule**

- (a) Sare ya shule hii ni rangi ya damu ya mzee kwa wavulana (Suruali) na wasichana (Sketi) ya mshono wa marinda madogo urefu chini ya goti wavulana isiwe modo au chupa, suruali, sketi na sweta ni ya damu yam zee.
- (b) Rangi ya Hijabu ifanane na rangi za shule, shati, sketi na T-shirt.
- (c) Sare ya michezo kwa shule hii ni suruali nyeusi na raba nyeusi waqvuana na wasichana sketi nyeusi na raba nyeusi.

- (d) T-shirt ya rangi ya ugoro au udongo
- (e) Viatu vya ngozi nyeusi vyenye kamba

**3.0** Aje na vifaa vya usafi: Jembe moja (01), Ndoo moja (01), Fagio Moja (01) na Fyekeo moja (01).

### **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais-Tawala za mikoa na serikali za mitaa (**OR-TAMISEMI**) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shuleni. Kushiriki kwa makini na kufanya maandalio ya jioni (**Peparation**).
- (c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya uwepo wa ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote uanafunzi wako katika shule hii.
- (e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na \
- (h) Kutunza mali ya umma.

**3.1** Makosa yafuatayo yanawezakusababisha kufukuzwa shule au kusimamishwa shule

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevywa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nakadhalika
- (e) Kupigana na kupiga
- (f) Kuaharibu makusudi mali ya umma
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa
- (h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
- (i) Kuo au kuolewa
- (j) Kutoa mimba
- (k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu
- (l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (m) Kuwa na simu ya mkononi

**4.1 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi**

- (a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- (b) Fomu ya melekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- (c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**Karibu katika shule yetu**

.....

**Bora F. Ndunguru**

**MKUU WA SHULE.**

## FOMU YA MAKUBALIANO

### SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi ..... Nimeyasoma na kuyaelewa maagizo pamoja na mwaongozo wa mabo ya kuzingatia shuleni. Ninaipokea nafasi hii niliyopewa na Taifa kuwa mwanafunzi wa kutwa Shule ya sekondari **FUNDIKIRA** . Ninaahidi kuzitekeleza Sheria na Kanuni za shule na kuzingatia masomo yangu kama inavyotakiwa, kinyume chake nichukuliwe hatua zinazostahiki.

Sahihi .....

Tarehe .....

### SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi ..... mzazi/mlezi wa .....

Nimeyasoma na kuyajadili na mwanangu maagizo haya. Nimekubali nafasi hii aliyopewa motto wangu na nitatimiza mahitaji yake yote kama mwanafunzi wa kutwa. Aidha nitahakikisha muda wote anazingatia sheria na taratibu za shule.

JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI ..... SAINI.....

KATA/KIJIJI ..... MTAA/KITONGOJI.....

NAMBA YA SIMU ..... TAREHE .....

### MWISHO

Ni tumaini letu kwamba mwanao atafurahia na kujivunia shule yake mpya. Hivyo tunamkaribisha na kumtakia mafanikio mema. Kwa kukubali nafasi hii tujazie Fomu ya Makubaliano na uchunguzi wa Hospitali ili mwanao aje nazo siku ya kuripoti shule.

.....

Bora F. Ndunguru.

MKUU WA SHULE

**PRESIDENT'S OFFICE (PO)**  
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**  
**FUNDIKIRA SECONDARY SCHOOL**  
**P. O. BOPX 799. TABORA.**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

This form must be completed by Government MEDICAL Officer

Student's full name: .....

Present age: .....

Blood test: .....

Stool examination: .....

T.B test: .....

Asthma: .....

Eye disorder:.....

Nose disorder: .....

Ear disorder : .....

Skin disease: .....

Anemia: .....

Chest: .....

Operations : .....

Serious accidents: .....

Any other infection diseases

ADDITIONAL INFORMATION e.g Physical defects or impairment, chronic or family diseases  
e.t.c

.....  
.....

I certify that I have personally examined Mr/Miss .....  
And found him.her fit/unfit to pursue studies.

Signature .....

Designation .....

(official rubber stamp)